# UKAMILIFU NDANI YA KRISTO

*Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu (Mt. Matayo 5:48).*

Ndugu, sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika, ila natenda neno moja tu, nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele, nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika kristo Yesu. Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo na hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu atawafumulia hilo nalo. Lakini, hapo tulipofika na tunaenda katika lilo hilo. (Wafilipi 3:13-16).

Siri ile iliyofichwa tangu zamani zote na tangu vizazi vyote, bali sasa imefunuliwa kwa watakatifu wake, ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu, ambaye sisi tunamhubiri habari zake, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika kristo. Nami najitaabisha kwa neno hilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu (Wakolosai 1:26-29).

Ndugu Branham aliulizwa kuhusu maandiko ya Waefeso 4:11 mpaka 13. Tunapata ukamilifu wote kwa njia ya kanda, au inatupasa kuwa hapa ambapo karama za Roho zinatenda kazi kupitia huduma mbalimbali za Kanisa kutusaidia kutukamilisha sisi? Mioyo yetu imeamini neno lote la Mungu.

Hapana. Wanataka kuja hapa Kanisani kwa ajili ya kukamilishwa. Hapa Kanisani tunapata ushirika mmoja kwa mwingine, lakini ukamilifu unakuja kati yetu na Mungu. Damu ya Yesu Kristo ndiyo inayotukamilisha sisi kwa Roho Mtakatifu.

Kwa hiyo tuna baadhi ya karama zinazotenda kazi kati yetu, na tutafurahi sana kushirikiana na yoyote miongoni mwenu, ambaye ana njia, kwamba unafanya kazi, au unataka kuja na kuwa na ushirika na sisi, chochote tuwezacho kufanya, tunafuraha sana juu ya hilo lakini sasa ule ukamilifu, unatoka kwa Kristo. [1]

Sasa: kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie (ukamilifu) utimilifu ..(Waebr. 6:1).

Nampenda Paulo anaposema mambo hayo. Paulo kamwe hakuwa mtu anayependa kukaa mahali pamoja kwa muda mrefu, alitaka aendelee kwenye kilindi. Wakati mmoja katika maandiko alisema “Tukiyasahau yaliyo nyuma, nakaza mwendo ni



kuya chuchumilia yaliyo mbele na kaza mwendo kwenye mwito mkuu” Unaona, anaendelea kukaza mwendo (Wafilipi 3:13-16). Hapa alisema. Sasa tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya kristo ……… (alikuwa ni nani, alikuwa na nini)…..tuendelee kwenye ukamilifu ……”

Kwanza tulitaka kujua “tunaweza kuwa wakamilifu?” Na tunaona katika maandiko, Matayo5:48, kwamba yesu alisema kuwa tunapaswa kuwa wakamilifu kama Mungu alivyo, au hatutaweza kuingia.

Halafu tunaona kuwa sisi sote tumezaliwa katika dhambi, na kuumbwa katika uovu, tumekuja duniani tukisema uongo. Na hakukuwa na kitu chochote kizuri juu yetu (Warumi 3:9-18). Kwa namna gani sasa twaweza kuwa wakamilifu?

Sasa, hapa tunaona hili (juu….. kusoma, kuchukuwa maandiko na maandiko) kwamba Yesu, kwa sadaka moja, alikamilisha milele kanisa lake. (Waebr. 10:14) kwa hiyo sasa sisi ni wakamilifu kupitia kristo (Warumi8:1). Na Kwa kupitia Kristo hatuhukumiwi (Yohana 11:25-26).

Hatutakufa kamwe kupitia Kristo. Tumepoteza mauti na kuona uzima kupitia Kristo, siyo kupitia Kanisa lolote, siyo kupitia dhehebu lolote, siyo kupitia vitu vya ajabu ajabu siyo kupitia kunena kwa lugha siyo kupitia kupiga makelele, siyo kupitia kutetemeka, siyo kupitia kucheza katika Roho, lakini ni kwa neema!
(Waefeso 2:8-9). [2]

Paulo alisema, “Natuweke kando mambo yote sasa “(Waebr. 6:1-3). Hiyo ni sawa, lakini tutafanya hivi. Tutawabatiza watu, na kuweka mikono juu yao kwa ajili ya uponyaji wao na kadhalika.

Tunaweza kuchukua mstari kwa mstari, kila kimoja ya vitu hivi. Ubatizo mmoja. “Waefeso 4:4-6. Tunaamini kwamba kuna ubatizo. Tunaamini katika ufufuo wa waliokufa, hakika, tunaamini Yesu alikufa na akafufuka tena. Tunaamini hilo, kuwawekea wagonjwa mikono, hiyo ndio lilivyosema, “Ishara hizi zitafuatana nao waaminio. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa watapata afya”. (Marko 16:18). Tunaamini hilo lakini ni nini? Paulo alisema, “hizo zote ni kazi nilizokupa”. Ni kitu kile unachofanya. Sasa natwende kwenye ukamilifu Oh, jamani.

Tunakuja kwenye ile maskani au (jengo), siyo msingi, ni ile maskani (jengo) maskani yenyewe. Huo ndio msingi. Sheria, na ile haki na kule kujiunga na Kanisa, na kubatizwa na kuwekewa mikono. Hizo ni taratibu za Kanisa lakini sasa natwende kwenye ukamilifu. Na kuna mmoja tu aliyekamilika, huyo ni Yesu.

Sasa, 1Kor. 12. Tunaingiaje katika huo mwili? Kwa kupeana mikono? Hapana, bwana. “kwa kujiunga na Kanisa?” Hapana bwana, kwa kubatizwa kinyume nyume, au mbele? Katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu? Kwa Jina la Yesu Kristo? Jina la Rose Sharon, ua la uwandani, nyota ya asubuhi? Chochote unachotaka? Hilo halina uhusiano na hilo, hilo ni jibu tu la dhamiri safi mbele za

Mungu (1Petro 3:20-21). Na bado tuna zoza na kuchemka, na kubishana, na kutengana na kufanya tofauti. Hiyo ni sawa. Lakini hizo zote ni kazi mfu.
Tunaenda kwenye ukamilifu.

Hayo ni mambo niliyofanya. Mhudumu amekubatiza wewe, kama amekubatiza kwa mbele, kwa nyuma, au mara tatu, mara nne au mara moja au vyovyote alivyofanya, hilo halina uhusiano na hilo. Unabatizwa tu kuwa mshirika wa Kanisa tu, kuthibitishia kanisa unaamini kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo.

Kule kuweka mikono kuponya wagonjwa, hilo ni zuri sana lakini yote ni ya kiasili na huo mwili utakufa tena kwa hakika sana kama vile hakika ya kuwa unaishi. Utakufa tena. Sasa, natuweke kando mambo haya yote na twende kwenye ukamilifu.

Kwa namna gani tunapata ukamilifu? Hicho ndicho tunachotaka kujua. Kristo amekamilishwa. (Waebrania5:7-8), Mungu ameweka juu yake maovu yetu sisi sote. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake. Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona (Isaya 53:4-7). Huo ndio mwili tunaotaka tunao taka kuingia ndani yake. Huo ndio mwili kwa nini? Kama uko ndani ya huo mwili, hutaona hukumu kamwe (Yohana 5:24), Hutaonja kifo kamwe uko huru kutoka na mauti yote, hukumu, dhambi na kila kitu chochote, unapokuwa kwenye ule mwili.

“Unaingiaje ndani yake, mhubiri? Kwa kujiunga na mashani hii?” Bado utakuwa umepotea. Huwezi ukajiunga nao kwa vyovyote, hatuna kitabu chochote. Tunaingiaje katika huo? Kwa kujiunga na Kanisa fulani? Hapana, bwana. Unaingiaje katika huo? Unazaliwa katika huo (1Petro 1:23), kwa maana katika Roho mmoja sisi tulibatizwa kuwa mwili mmoja (1Kor. 12:13).

Kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, tunabatizwa ndani ya ule mwili, na tunakuwa huru na dhambi. Mungu hakuoni wewe tena, anamuona Kristo tu. Na unapokuwa kwenye ule mwili, Mungu hawezi kuuhukumu ule mwili. Amekwisha kuuhudumu. Amechukua hukumu yetu na kutukaribisha ndani. Na kwa Imani kwa njia ya Neema tunatembea na kukubali kusamehewa kwetu. (Waefeso 2:8-9). Na Roho Mtakatifu anatuleta sisi katika ushirika na Yeye. Na hatuendi tena kwenye mambo ya dunia, lakini tunatembea katika Roho. Tumehuishwa, Neno limekuja kwetu. Amekufa badala yangu. Nimefanywa mzima. Niko hapa ambaye nilikuwa nimekufa katika dhambi na makosa, nimefanywa mzima (Waefeso 2:1-5). Shauku yangu yote ni kumtumikia Yeye. Upendo wangu wote ni kwake kutembea kwangu kote natoka kuwe kwa Jina lake ili kwamba popote niendapo, chochote nifanyacho, Ninamtukuza Yeye kama ninawinda, kama ninavua, kama ninacheza mpira …chochote nifanyacho lazima niwe “Kristo ndani yangu” katika maisha ambayo yatawafanya watu wawe na kiu ya kuwa hivyo: Siyo mpayukaji, msengenyaji, na anayezoza juu ya Makanisa. Unalipata hilo? Kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa katika ule mwili, na nionapo damu nitapita juu yako “(Kutoka 12:13) [3]



Zile hatua za kusudi lake la milele alilokuwa nalo katika siri yake limefunuliwa sasa. Angalia sasa, bado kuna hatua tatu za ukamilifu. Kama vile anavyoikomboa dunia, kadhalika ndivyo anavyolikomboa Kanisa lake. Anakomboa watu katika hatua tatu. Sasa, angalia, moja ni kuhesabiwa haki kama luther alivyohubiri, mbili kutakaswa kama weslay alivyohubiri, tatu, ubatizo wa Roho mtakatifu. Hiyo ni kweli. Halafu unakuja unyakuo. [4]

Tunataka ninyi muokolewe, marafiki. Tunataka ninyi mjazwe. Kumbuka, umeokolewa, kweli. Unapomkubali Kristo umeokolewa, lakini hujabadilishwa mpaka umepokea Roho Mtakatifu. Sasa unajua hilo, hiyo ni kweli.

Yesu alimwambia Petro usiku ule wa kusalitiwa …. Yeye akiwa tayari ameokolewa. Alisema, “sasa, baada ya kuongoka (kubadilishwa) waimarishe ndugu zako, “(Luka 22:31-32). Hiyo ni kweli. Oh, hakika. Unamkubali Kristo kama mwokozi wako. Lakini unapoongoka ni pale unakuwa aliyebadilishwa hasa. Hiyo ni sawa. Alikuwa hajabadilishwa bado. Alilaani mbele za Bwana, na akamkana Yeye, na kila kitu. Lakini baada ya kuongoka….. “Baada ya kuongoka kwako, imarisha ndugu zako”.

Hiyo ni kweli. Je hiyo ni sawa? Iwavyo vyote ni vile maandiko yasemavyo. Na hiyo inalifanya liwe sahihi. Yesu alimuambia petro, ambaye alimfuata yeye, na kutoa mapepo (Matayo 10:1), na akafanya miujiza, na kila kitu, alisema, “Bado hujaongoka bado. Lakini baada ya kuongoka, hapo sasa imarisha ndugu zako.” Hiyo ni sawa ni kweli. [5]

Unapotenganishwa kutoka kwenye muungano wako wa kwanza kwa kifo cha kiroho (Warumi 7:1-6). Sasa, umezaliwa mara ya pili, au umeolewa tena kwenye muungano mpya wa kiroho, siyo maisha yako ya asili ya mambo ya dunia, bali ni ya uzima wa milele. Ile chembe iliyokuwa ndani yako pale mwanzo, imekuona.

Sasa kitabu chako cha zamani kimefutwa pamoja na muungano wako wa zamani. Sasa, jina lako katika kitabu cha zamani umehamishwa sasa, unasema “unamaanisha kuniambia kwamba kitabu changu cha zamani….. “Mungu amekiweka kwenye bahari ya usahaulifu. (Mika 7:18-19). Unasimama mkamilifu mbele za Mungu.

Sasa, jina lako liko katika kitabu kipya, siyo katika kitabu cha uzima, lakini kitabu cha uzima cha mwanakondoo. Kile mwanakondoo alichokomboa, siyo kile kitabu cha zamani cha muungano wako wa asili, bali ni Bibi Arusi mpya. Haleluya! Maisha yako mapya yako katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo, Hati yako ya ndoa (Halleluya) mahali ambapo ile chembe ya kweli ya milele inashikilia kutoka mwanzo.

Sasa, siyo tu umesamehewa, bali umehesabiwa haki utukufu, kuhesabiwa haki Warumi 5:1 ilisema, “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani …. Angalia hilo Neno halimaanishi kusamehewa. Hilo Neno linamaanisha kuhesabiwa

haki. Halimaanishi umesamehewa, kwa mfano, umesikia kwamba nimelewa na nikaenda kufanya vitu viovu na vyote, sasa unakuja karibu na kusema nami…… ukaona kwamba sikufanya vitu hivyo. Sasa unakuja karibu na kusema, "Ndugu Branham, ninakusamehe wewe." Unanisamehe mimi? Sikulifanya hilo toka mwanzo.

Sasa kama nimelifanya ninahatia, ila unaweza kunisamehe mimi na nisiwe na hatia, ila bado sihesabiwi haki, kwa sababu nililifanya kwa uhakika. Lakini Neno "kuhesabiwa haki," ni kama hujafanya hilo kamwe. Amen. Halifikiriwi kabisa. Linafanyikaje? Katika kitabu cha Mungu cha bahari ya usahaulifu, kitabu chako cha zamani na ndoa vimetalikiwa na vimekufa na haviko kamwe hata kwenye kumbukumbu za Mungu. Amen. Umehesabiwa haki. Basi tukiisha kuhesabiwa haki……. Ilikuwa ni laana….. Ulikuwa umelaaniwa, hujafanya hivyo kwa kuanzia ule muungano wa zamani uko katika bahari ya Mungu ya usahaulifu. Hukuolewa katika hilo tangu mwanzo, Yeye, Bwana arusi anaibeba/anaichukua aibu yako Yeye mwenyewe anachukua mahali pako. Alichukua mahali pako, kwa maana ulikuwa umechaguliwa kimbele na yeye kuwa katika Bibi Arusi wake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Biblia ilisema hivyo. Wewe ni mbegu iliyochaguliwa kimbele (Wagalatia 4:6-7).

Umekuwaje kuishi/kufanya haya? Ulidanganywa kuingia kuyafanya na ndoa yako ya kwanza….. kwa mzazi wako mzinzi Hawa. Siyo kosa lako mwenyewe. Ni kwa uzazi wako wa asili, ulikuja baada ya Hawa, aliyetenda uzinzi. Hiyo ndiyo sababu ulizaliwa ukiwa mzinzi. Ulikuwa ni mdhambi kwa kuanzia. Hiyo ni kweli. Ulidanganywa katika hilo. Hapana, siyo kosa lako. Hukulifanya kamwe, kwa sababu ile chembe ndogo iliyokuwa ndani yako, ilikuwa iwe wewe kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu. Mungu aliweka jina lako katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo.

Yeye Bwana arusi ameichukulia mbali aibu yako na kuiweka kwenye bahari ya usahaulifu kwa kuoshwa kwa maji katika Neno na Damu ya uzima. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

Mume wako wa kwanza ambaye alikuoa, dunia, Bwana Arusi aliyepakwa mafuta, ambaye alikukusudia kimbele, amekuosha wewe kwa kuoshwa kwa maji ya Kanisa? Hiyo haisikiki kuwa sahihi si ndiyo? Unaweza ukalipata hilo katika almanaki, lakini siyo katika Biblia ya Mungu. Kwa kuoshwa kwa maji katika Neno na Neno (Waefeso 5:25-27). Unasimama ukiwa umehesabiwa haki kana kwamba hujalifanya hilo tangu mwanzo.

Huu ni ujumbe wangu kwa Kanisa sasa. Mmesimama. Kama mmesimama katika Neno la Mungu na una neno la Mungu, Kila amen, kila nukta, kila kitu kidogo. Unasimama wapi? Ninajaribu kuwaambia ninyi. Tokeni kwenye hayo makapi na mje hapa katika ngano ambapo unaweza kukomazwa mbele za jua. Ninasikia kule kuja kwa mashine ya kuvunia. Mmesimama wakamilifu, kuhesabiwa haki kana



kwamba hujalifanya hilo kwa kuanzia. Haleluya. Zungumza juu ya kutoa shukrani. Ninajiskia vizuri sana. Ninashukurani kwa hilo zaidi ya kitu chochote kile nijuacho.

Wewe ni msafi, Bikira, Bibi arusi asiye na dhambi wa mwana wa Mungu aliye hai. Kila mwanaume na mwanamke ambaye amezaliwa kwa Roho wa Mungu, na kuoshwa katika damu ya Yesu Kristo, na kuamini kila Neno la Mungu, anasimama kana kwamba hajatenda dhambi kamwe hata mara moja. Umekamilika. Damu ya Yesu kristo.

Kama ningepaswa kufa asubuhi, na mtu kuchukua mahali pangu, siwezi kufa kwa ile dhambi. Mtu fulani amechukua mahali pangu. Na Yesu, aliye Neno amechukua mahali pangu. Alikuwa mimi, mwenye dhambi, ili kwamba niwe Yeye, lile Neno. Amen. Hebu nishikilie kwa uaminifu kwa hilo, siyo Kanisa, Neno, Amen.

Oh, ule muungano wa kristo katika Kanisa lake sasa, wakati mwili unafanyika Neno na lile Neno linafanyika mwili. Linadhihirishwa, linathibitishwa, kile ambacho Biblia ilisema kingetokea katika siku zetu, kinatokea siku kwa siku, kwa nini, vinajazana kwa haraka sana nje kule jangwani, na mambo yanayofanyika, ambayo hata nisingeweza kuyastahimili. Tuko karibu na kuja kwa Yesu ili kuungana na Kanisa lake, mahali ambapo lile Neno linakuwa Neno.

Roho Mtakatifu anaita kuchunguza mioyo …. Umesimama ukiwa umekamilika. Kamwe hujatenda dhambi hata mara moja. Mungu hata hajui …..iko katika bahari ya usahaulifu. Hujafanya hivyo kamwe. Ulishitakiwa hivyo na mshitaki, lakini hasa kutoka mwanzo ulikuwa umechaguliwa kimbele kuwa mwana au binti wa Mungu. Umesimama pale ukiwa umeoshwa, na kitabu chako cha zamani cha kukutaliki kimewekwa mbali nacho kimekufa, hakika hakipo tena hata katika mawazo ya Mungu. U bibi arusi Bikira wa Kristo, aliyeoshwa katika Damu ya Kristo. Damu ya thamani, Bikira, asiye na dhambi, Mwana wa Mungu akiwa amesimama pamoja na Bibi arusi safi aliye Neno lisilochanganywa, ambaye ameoshwa kwa maji ya damu yake mwenyewe ambayo imekuwa mwili na imedhihirishwa kwamba akuchukue wewe, ambaye ulichaguliwa kimbele kifuani mwa Baba kabla ya ule Mwanzo, sawa na vile alivyokuwa………..

Alikuwa ile sifa kubwa ya Mungu iliyoitwa, Upendo. chochote ulicho, ni watumishi wa Mungu chochote atakacho Mungu afanye, mahali pako ulipo ….. Mungu aliweka katika Kanisa wengine ni mitume, manabii, waalimu, wachungaji (Waefeso 4:11-16) Aliweka hilo kwa tabia yake mwenyewe ya kujua kimbele. Na ulikuwa hivyo kwa kuanzia. Ndoa yako ya kwanza ilibatilishwa. Hujafanya hilo hata hapo kwanza, kwa sababu kuna kitu kimoja tu kiwezacho kufanya hivyo na hilo lingekuwa ni Mungu kushuka chini, mwenyewe, na achukue mahali pako katika umbile la mwana wa Mungu, Yesu Kristo, na kukuosha wewe kwa maji …. Kukuosha kwa maji katika Neno. Lile Neno, siyo lile dhehebu, lile Neno limekuosha wewe. Lakini kama hutasimama katika maji ya neno, utaenda kuoshwa vipi? Bado una madoa doa kama Hawa alivyokuwa.

"Oh, mpendwa mwanakondoo aliyetufia, Damu yako ya thamani haitapoteza nguvu mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa liokoke lisitende dhambi tena" (1Yohana 3:4-6,9; 5:18).

Dhambi ni nini? Dhambi ni kutokuamini (Yohana 16:7-11), kutoamini katika nini? Neno. Kutoamini Mungu, ambaye ni Neno. Safi lisilochanganywa (Oh, halleluya), linaondoka karibuni kwenda mawinguni. Amen. Linasimama tayari ….. Fikiria, mavazi yako yakiwa yameoshwa kwa maji ya damu imwagikayo ya Neno. Lile Neno limekuwa damu. Lile Neno limetoa damu kwa ajili yako, na umeoshwa kwa Neno linalotoa damu. Neno linavuja damu, uhai wa Mungu ndani ya Neno, na Neno lilivuja damu kwa ajili yako, kwamba uweze kutakaswa na uchafu wote wa uasherati na usafishwe na kutakaswa kwa kuoshwa kwa damu katika Neno hilo unaifanya akili yako na moyo wako vikae kwa Mungu na katika Neno lake [6]

Sasa, tunaona maisha haya yanashikilia aina zote za uovu, kwa hiyo, maisha yale yajayo hayatakuwa ni hayo. Haya yanatamaa, na magonjwa na kifo, kwa sababu ya nini? Siyo kao/nyumba aliyoenda kutuandalia. Hii ni nyumba ya wadudu. Ni wangapi wanajua nyumba ya wadudu ilivyo? Hakika vema. Hiyo ndiyo nyumba unayoishi ndani yake. Nyumba ya wadudu ni ile ambayo wanaweka watu wote walio wagonjwa. Vema hivyo ndivyo dhambi ilivyofanya kwetu, kutuweka sisi katika nyumba ya dunia nyumba ya wadudu. wasingemruhusu mtu yoyote aje katika nyumba ya wadudu, kwa sababu kuna aina zote za wadudu wabaya wanaoruka katika mazingira hayo, na watu watachukua wadudu hawa na watakuwa wagonjwa. Na dhambi imetuleta katika nyumba ya wadudu ya shetani (Warumi 7:22-25)

Oh, lakini ile nyingine inaitwa nyumbani mwa Baba yangu "Nitaenda na kuwaandalia mahali kwa ajili yenu, niwatoe kutoka kwenye nyumba hii ya wadudu na kuwaingiza katika nyumba ya Baba yangu." (Yohana 14:1-3). Amen. Unaona hilo, kuwachukua ninyi mtoke katika nyumba hii ya wadudu ya zamani ya duniani……

Ameenda kuandaa mahali, mahali pa kamilifu, ambapo hakuna uovu pale, hakuna magonjwa pale, hakuna uzee pale, hakuna kifo pale, Ni mahali pakamilifu panapokuita wewe kwenye ule ukamilifu, na unapaswa uwe mkamilifu ili uweze kufika pale. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema, "Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu". Na ni ufalme uliomkamilifu, kwa hiyo lazima iwe ni watu wakamilifu wanakuja, kwa sababu inabidi usimame na uolewe na mwana wa Mungu aliyemkamilifu, na unapaswa kuwa Bibi Arusi aliyemkamilifu. Sasa utawezaje kufanya hivyo na kitu kingine chochote bila Neno kamilifu la Mungu, ambalo ni Maji ya furaha na ambayo yana tuosha kutoka kwenye dhambi zetu. Amen. Hiyo ni sawa. Damu ya Yesu Kristo …… Fikiria hilo kule kuvuja. Neno lenye damu (Amen) ile damu, lile Neno la Mungu linadondosha damu ili kumuosha yule Bibi arusi. Amen. Ndiyo, Bwana, anasimama mkamilifu, bikira, asiyejichanganya, Hajatenda dhambi hata pale mwanzo. Amen. Yeye alitegewa na kunaswa katika hilo. Tunaona, kuna makao nyumbani kwa Baba ambapo ameenda kuandaa. [7]



**Nukuu za Kiingereza**

[1] Maswali na majibu COD uk. 1109-1110, Swali na 355
[2] Waebrania sura ya 6 uk 206 – 207, Aya 244 – 249.
[3] Waebrania sura ya 5 na 6 sehemu ya 1 uk. 184 – 186, Aya 104 – 107, 113 – 118.
[4] Ni nani huyu Melkizedeki aya 113.
[5] Mungu katika urahisi (63 – 0412E), Aya 138 - 139.
[6] Muungano usioonekana uk. 32 – 39.
[7] Mambo yatarajiwayo kuwa Aya 61 – 62.

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 156 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.
(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*

.